JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAMISEMI

Shule ya Sekondari ya Wasichana Maswa,

S.L.P 60 MASWA

Mkuu wa shule:- 0757672502

Makamu mkuu wa shule 0756 301752

Matron 0766302668

Mzazi/Mlezi wa……

S.L.P……

……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MASWA HALMASHAURI YA MASWA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2018/2019

1. Nafurahia kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 20178/2019 tahasusi ya …….shule ya sekondari ya wasichana maswa. ipo umbali wa Kiometa 4 kaskazini Mashariki ya mji wa maswa.

   Kuna usafiri wa mabasi kutoka mjini Mwanza hadi maswa mjini. Pia kuna usafiri wa magari madogo madogo na mabasi kutoka Shinyanga mjini hadi Maswa. Watokao Singida , Arusha, Kilimanjaro,Dar, Morogoro, Dodoma nk kuna mabasi ya kukufikisha Maswa moja kwa mojaau shinyanga. Kuhusu usafiri wa gari moshi (treni) toka Dar es salaam, Dodoma,Tabora na Mwanza vituo vya kuteremkia ni Malampaka au Shinyanga mjini ,yapo magari madogo yakutoka malampaka hadi maswa mjini.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 03.07.2018 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 03.07.2018 isipokuwa kama itatangazwa vinginevyo. Mwisho wa kuriport ni tarehe 18.07.2018

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-
   (a) Sare ya shule

   Sketi mbili ndefu mpaka chini(Ifike kwenye kifundo cha mguu) rinda box mbele na nyuma kulia na kushoto mwa rinda box iwe na marinda manne, belt inchi mbili na isivaliwe chini ya kitovu.**Aina ya jora au kitambaa ni esteem namba 1 au 2.**

   (b) Juba/Shungi mbili nyeupe kwa waislamu zinazofunika kifua. Blauzi mbili nyeupe za tetron, mshono wa shati mikono mirefu kwa wakristo.

   (c) Tracksuit ya light blue na Tshirt ya taifa stars rangi ya blue kwa ajili ya michezo.

   (d) Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba visivyo na kisigino kirefu.

(e) Soksi jozi mbili nyeupe ndefu sisizo napambo lolote au mchanganyiko wa rangi nyingine.

(f) Sweta ya rangi nyeusi yenye mchirizi mweupe shingoni, mikononi, na mwishoni mwa sweta kama inavyoonekana kwenye picha ukurasa wa 8, shingo iwe ya V.

(g) Gauni mbili rangi dark blue rinda box mbele na nyuma ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu.Shingo iwe ya mviringo kola yenye mpasuo mbele ya light blue , mikono mifupi ya shati na iwe na binding ya light blue **kwa wakristo. kwa waislamu**gauni iwe na mikono mirefu yenye binding ya light blue, pia wawe na juba/shungi ya light blue. **Aina ya jora au kitambaa ni esteem namba 1 au 2 kwa wanafunzi wote. tetron nzito light blue kwa ajili ya juba, binding za gauni mikononi na kwenye kola ya shingoni.**

(h) Tishet ya light blue yenye kola zenye michirizi yenye rangi nyeusi na mikono pia kama inavyoonekana kwenye picha

(i) Tai mbili nyeusi yenye mchirizi mweupe.

3. ADA NA MICHANGO YA SHULE

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs70,000, unaweza kulipa kiasi cha Tshs 35,000 kwa muhula au kulipia ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Na**30810000683**Jina ni **Maswa GirlsRecurrent Account** katika Benki ya **NMB** (**TAFADHALI ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI KWENYE PAY SLIP**)

(b) Michango mingine ni :-

i. Shilingi 15,000/=kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000=/ kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule
vi. Shilingi 10,000=/ kwa ajili ya huduma ya kwanza Tshs. 5,000/= na Bima ya Afya CHF kikaya)
vii. Shilingi 20,000/= mitihani ya kupima *mock*.
viii. Shilingi 10,000= kukodisha godoro kwa muhula.
ix. Fedha ya tahadhari 5000/= (hairejeshwi)

NB: Aidha ada, michango ya kitambulisho na picha, taaluma,wapishi,walinzi na vibarua wengine, nembo,bima ya afya, mitihani na tahadhari iwekwe kwenye akaunti na **30810000683** Jina ni **Maswa GirlsRecurrent Account**. Mchango wa ukarabati wa samani ulipwe kwenye akaunti namba **30810000682**. Jina:- **Maswa Girls Secondary School Development.**

(c) Mahitaji mwanafunzi ambayo anapaswa kuleta shuleni ni :-

i. Ream ya karatasi 1 kwa (Mwaka).

ii. Dissection kit kwa wanafunzi wa biolojia.

iii. Scientific calculator.

iv. Mashuka pair 2,foronya 2, neti 1 vyote viwe na rangi nyeupe.

v. Sahani, bakuli na kikombe viwe vya udongo na kijiko.

vi. Ndoo mbili ndogo nyeupe. zenye mfuniko.

vii. Kwanja 1, Jembe 1, Reki 1, ufagio wa ndani 1, ufagio wa nje 1

4. **Wajibu wa mwanafunzi**

i. Kuamka asubuhi na mapema na kila unapohitajika
ii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
iii. Kuvaa sare ya shule wakati wote kuhudhuria masomo siku zote za masomo
iv. Kuepukana na utoro na uzembe,udanganyifuna uhuni wa kila aina
v. Kuwa na nidhamu ya hali ya juu mahali popote
vi. Kushiriki kikamilifu katika kazi za shule michezo na utamaduni
vii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo shuleni wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
viii. Kushiriki katika shughuli zote zinazokujenga kuwa raia mwema
ix. Mwanafunzi sharti aonekane nadhifu wakati wote
x. Mwanafunzi haruhusiwi kupaka kucha rangi,kupakaa rangi mdomoni na kutunza kucha ndefu wakati wote ukiwa shuleni unatakiwa kuzingatia wajibu wako kama mwanafunzi.Unatakiwa kudumisha amani,nidhamu,ushirikiano,utendaji kazi kwa heshima na kwa kila mtu,wanafunzi wenzako,walimu,wafanyakazi wasio walimu,wanakijiji na viongozi wote.

5. **Sheria na kanuni muhimu za shule**

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia busara(common sense)katika maisha yote awapo shule.
ii. Wanafunzi lazima wawe na heshima na utu kwa watu wazima na wengine na kati yao wenyewe.
iii. Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza na kuangalia mali ya shule ya yake binafsi.
iv. Wanafunzi hawaruhusiwi kufika nyumbani kwa walimu bila ruhusa ya matroni.
v. Ni marufuku kuingia katika nyumba za starehe kama vile Baa,dansi na nyumba za kulala wageni(Guest house).
vi. Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza mazingira ya shule ,madarasa,vyoo na vyumba vingine shuleni katika hali ya usafi.
vii. Matusi ya kusema au kuandika na ugomvi ni marufuku shuleni .
viii. Mwanafunzi ni lazima ahudhurievipindi kwa masomo yote.Aidha ni lazima kuhudhuria vipindi vya dini yake kila siku kadri ya ratiba iliyopangwa.
ix. Ni mwiko kwa mwanafunzi kujiunga na vikundi nyenye tabia mbaya popote pale na nje ya shule.

x. Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi shuleni kwa muda ulipangwa.
xi. Ni marufuku kupokea wageni wa kwako binafsi uwapo shuleni.
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule bila ruhusa.
xiii. Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele awapo darasani .
xiv. Mwanafunzi atunze nywele zake zikiwa fupi.Ni marufuku kuweka dawa (curl au relaxer) kwenye nywele.
xv. Ni marufuku mwanafunzi kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele ndefu.Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara,panki na kutinda nyusi za macho/usoni.
xvi. Mwanafunzi anapaswa avae sare wakati wote awapo shule na nje ya shule.
xvii. Urafiki wa mwanafunzi wa kike na kiume uwe ule wa kaka na dada.

6. **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.**
   i. Wizi.
   ii. Uasherati na ushoga.
   iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi kubeli na n.k.
   iv. Kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzake,mwalimu au mlezi wake.
   v. Kuharibu kwa makundi mali ya umma.
   vi. Kudharau Bendera ya Taifa.
   vii. Kuoa au kuolewa.
   viii. Kupata mimba kutoa mimba ndani na nje ya shule.
   ix. Kugoma,kuchochea migomo kuongoza na kuvuruga amani na usalama wa shule.
   x. Dharau au kukataa adhabu kwa makusudi .
   xi. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
   xii. Utoro wa muda mrefu hadi muda wa siku tisini mfululizo.
   xiii. Kosa lolote kubwa ambalo uongozi wa shule utaamua mwanafunzi anastahili adhabu kama hiyo .

Mwisho

Ni imani yangu kuwa utasoma kwa makini/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu karibu sana Maswa girls

wako

THE HEADMISTRESS
MASWA GIRLS' SECONDARY SCHOOL
P.o. Box 60
MASWA.

KUYUNGA JACKSON

MKUU WA SHULE

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

SEHEMU B: FOMU YA MAMBO BINAFSI (PERSONAL PARTCULARS) IJAZWE KWA HERUFI KUBWA

1. Jina la mwanafunzi …….
2. Tarehe ya kuzaliwa ……mwezi……mwaka……..
3. Uraia ……Kabila……..
4. Anuani kamili ya nyumbani(yaani wazazi/walezi
   ……
   ……
   ……..

Taja mahali ambapo mwanafunzi ataishi wakati wa masomo

5. Dini yake ……..…dhehebula ……
   Jina la Baba/ ……Hai/sio…….
   Jina la mama…….Hai/sio……..
   Kazi ya Baba……
   Baba /mama/Mlezi anaishi kijiji/mtaa……..wilaya…….….Mkoa……
   Namba za simu ya Baba/Mama/Mlezi…….
   Kama anatunzwa na mlezi uhusiano ulionao na mlezi wako……
   Taja tatizo la kiafya/maumbile ulilo nalo(onesha na ambatanisha kivuli cha cheti kama kipo……
6. Andika majina ya ndugu ambao watashughulikia matatizo ya mwanafunzi

NA	JINA LA NDUGU	ANUANI	NAMBA YA SIMU	UHUSIANO NA MWANAFUNZI
1				
2				
3				
4				

7. Maelezo ya nyongeza kama yapo :
   ……
   ……
   ……
   ……..

SEHEMU C: FOMU YA KUPIMWA NA DAKTARI

(Nenda na fomu hii kwa daktari/Mganga katika Hospital ya Mkoa au Wilaya ili akupime na kukujazia ipasavyo)

Shule ya sekondari Maswa
S.L.P 60,
MASWA
TAREHE……

Daktari/Mganga wa Mkoa wa mkoa/Wilaya

……

……

……

MEDICAL CERTIFICATE

1. Jina la mwanfunzi ……..

2. Kidato cha …….mwaka ……

3. Nimempima mtajwa hapo juu na amepatikana na ugonjwa wa …….na amepatiwa/hakupatiwa matibabu ipasavyo

4. Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona hawezi kuendelea na masomo ya sekondari kwa sababu (kwa wasichana tu)imebainika kuwa ana/hana mimba ya miezi ……

5. AFYA KWA UJUMLA

a) Kifua ……..
b) Macho…….
c) Akili……..
d) Kilema chochote (kitaje)……..
e) Mkojo……
f) Choo(stool)…….
g) Maradhi mengineyo(yataje)……
……
……

Jina la Daktari/Mganga ……..…….sahihi …….tarehe……

JAMUHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MASWA

S.L.P 60 MASWA, SIMIYU

KIAPO KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018/2019

Mimi……..niliyechaguliwa kuwa……ninaahidi kuwa nitakuwa mwaminifu kwa walimu, wafanyakazi wasio walimu,wanafunzi wote na jumuiya nzima ya maswa girls . Nitatii sheria za shule , sheria za jamuhuri ya muungano wa Tanzania zilizowekwa na zitakazowekwa, nakiri kwa moyo wangu wote kuwa nitasema kweli daima.

Nitaitumikia jumuiya ya sekondari ya wasichana maswa kwa kadri ya uwezo wangu wote.

MUNGU NISAIDIE

…… ……

Saini ya mwanafunzi Saini ya mkuu wa shule

Tarehe…… Tarehe……..

SHAMBA DRESS KWA WANAFUNZI WA KIKRISTO. KWA WANAFUNZI WA KIISLAMU NI GAUNI HII HII, ILA IWE YA MIKONO MIREFU YENYE BINDING YA LIGHT BLUE, PIA

SARE YA DARASANIO KWA WANAFUNZI WA KIISLAMU

SARE YA DARASANI KWA WANAFUNZI WA KIKRISTO